*Journal of African Interdisciplinary Studies (JAIS)*: **ISSN 2523-6725** (online)
**October 2024 Vol. 8, No. 10**
**Citation**: Jeptanui, S & Gakuo, J. K. (2024). Usawiri Wa Changamoto Zinazowakumba Wazamilifu Katika *Ubabe. Journal of African Interdisciplinary Studies,* 8(10), 405 – 420.

# Usawiri Wa Changamoto Zinazowakumba Wazamilifu Katika *Ubabe*

Na

Sarah Jeptanui na Joseph Kariuki Gakuo
Corresponding author email: sarahjeptanui24@gmail.com

**Ikisiri**
Makala haya yanashughulikia changamoto zinazowakabili wazamilifu yaani, wasomi wa shahada ya uzamili na wale wa uzamifu katika vyuo vikuu nchini Kenya kama ilivyosawiriwa katika Tamthilia ya Ubabe (Gakuo: 2020). Lengo kuu ni kubainisha namna mwandishi wa tamthilia hii teule alivyofanikiwa kusawiri uhalisia wa changamoto zinazowakumba wasomi hao katika tamthilia ya Ubabe. Makala haya yanachunguza mazingira ya masomo katika vyuo vikuu nchini Kenya kama yanavyoakisiwa katika tamthilia ya Ubabe na maudhui ya Ubabe yanavyojitokeza miongoni mwa viongozi mbalimbali vyuoni, na athari zake kwa wasomi hao wa ngazi za juu. Tumechochewa na sababu kwamba masomo ya shahada za juu (uzamilifu) ni kiungo muhimu cha taaluma kwani, wasomi hao ndio wataalam wa kesho. Kwa hiyo, uzamilifu ni mhimili wa uendelevu wa kiakademia na kitaaluma kwa jumla. Changamoto zinazowakumba hivyo basi huenda zikawa tisho kubwa inayotinga mstakabali wa taaluma anuai zinazoendelezwa katika vyuo vikuu nchini na kwingineko duniani. Uchunguzi wetu umeongozwa na nadharia ya uhalisia ambayo kimsingi, huthamini kazi ya fasihi kama kioo cha hali halisi ya jamii. Pamoja na kuwa zao la jamii, fasihi pia ni kiakisi cha ukweli unaodhihirika katika maisha ya jamii katika ulimwengu halisi. Tamthilia hii ni tamthilia ya hivi punde ya Kiswahili inayohalisi mazingira ya usomi ya vyuo vikuu na haijfanyiwa uchunguzi wa kina. Ni matumaini yetu kwamba makala haya yatakuwa muhimu kwa watafiti wengine na wadau wa fasihi kama kihamasisho cha kuchunguza kazi za fasihi kwa mtazamo wa uhalisia ili kuhakiki dhamira za watunzi kwa manufaa ya hadhira kusudiwa na kwa manufaa ya hadhira pana ya wapokezi wa fasihi ya Kiswahili.

**Maneno Muhimu (keywords):** Ubabe, Uzamifu, Uzamili, Fasihi and Taaluma

*Journal of African Interdisciplinary Studies (JAIS)*: ISSN 2523-6725 (online)
October 2024 Vol. 8, No. 10
**Citation**: Jeptanui, S & Gakuo, J. K. (2024). Usawiri Wa Changamoto Zinazowakumba Wazamilifu Katika *Ubabe*. *Journal of African Interdisciplinary Studies*, 8(10), 405 – 420.

**Usawiri Wa Changamoto Zinazowakumba Wazamilifu Katika *Ubabe***

Na

Sarah Jeptanui na Joseph Kariuki Gakuo

## 1.0 Tamthilia ya U*babe*

Ubabe ni tamthilia ya hivi punde ya Kiswahili ambayo mtunzi wake ni Gakuo Joseph Kariuki.Imetungwa mwaka wa 2020. Mtunzi anaangazia suala la elimu ya kiwango cha juu yaani, uzamili na uzamilifu katika vyuo vikuu nchini Kenya na kwingineko duniani. Kutokana na tabaruku yake, mtunzi anadhamiria kazi hii kwa hadhira ya wasomi wake wazamili na wazamifu. Anasema: "Kitabu hiki nakitabaruku kwa wanafunzi wangu Wazamili na Wazamifu na wengine wote watamanio kubobea katika lugha ya Kiswahili." Hapa ni Dhahiri kwamba mtunzi ni mhadhiri wa chuo kikuu na kwa sababu aisifue mvua imemnyia, tunahisi kwamba anaandika kutokana na tajriba yake kwanza kama msomi wa shahada za juu, na pili, kama mhadhiri wa chuo kikuu.

Inadhihirika kwamba msimamo wa mtunzi huyu ni kupinga na kupigana na uhasama unaowakumba wasomi hawa wa kiwango cha juu vyuoni. Mawazo yake yanadhihirika kupitia kwa wahusika wakuu mbalimbali ambao ni Mahiri na Mwanamkiwa pamoja na wahadhiri wema idarani wakiongozwa na Prof. Mzee. Hadhira yake ya upokezi wa kazi yake pia inadhihirika kupitia kwa wahusika wake. Takribani wote ni wanachuo. Mtunzi ametumia wahusika wa aina mbili kuu hususan wanafunzi wazamilifu na wakufunzi wa vyuo vikuu. Wazamilifu hao ni pamoja na : Mahiri; Mwanafunzi mzamifu tena kiranja wa darasa la wazamifu na shahada za juu idarani, Mwanamkiwa; Mwanafunzi mzamili, Athumani, Mwanafunzi mzamili, Maridhia, Mwanafunzi mzamifu, Mwangwi, Mwanafunzi mzamili na Makini; Mwanafunzi mzamili. Kuna pia wanafunzi ambao wanatajwa tu katika tamthilia na ambao hatuwaoni ila tunawasikia tu. Wote hawa inadaiwa kuwa ni wale wanaopendelewa na Mbabe na kundi lake la uongozi.Wahusika hao ni pamoja na Labeka naWaladi.

Wahusika wahadhiri nao wanaweza kugawika katika mapote mawili yaani wema na waovu. Wema ni Pamoja na Profesa Mzee; Mhadhiri mkuu ambaye ni profesa kamili idarani aliyefanya kazi kwa muda mrefu,Mwalimu Mbasi; Mhadhiri ambaye haungi mkono sera za mwenyekiti, Daktari Kigogo; Mhadhiri idarani aliye mcheshi na anayependa kazi yake, Profesa Wasta; Mhadhiri anayependa kuwashauri wanafunzi katika shahada za juu na Daktari Mkombozi; Mhadhiri idarani. Wote hawa ni wahusika wema na ambao wanafanya kazi yao vyema na kwa roho safi bila ushindani wala kinyongo kwa wanafunzi wazamilifu ambao ndio wateja wakuu wa chuo kikuu.

Wahusika waovu na ambao kwa bahati mbaya ndio wenye kusema idarani (yaani walio na madaraka na nyadhifa zauongozi), wanaongozwa na Daktari Mbabe; Mwenyekiti wa idara, Daktari Mzushi; Mhadhiri idarani anayeunga mkono sera za mwenyekiti, Daktari Makongoro; Mhadiri na mwenyekiti kamati ya mgao wa kazi idarani, Profesa Makuruhu; Mhadhiri mwenyekiti wa kamati ya jarida la idara, Mwalimu Mgobo; Mhadhiri mwenyekiti wa kamati ya maslahi idarani, Mwalimu Mwambi; Mhadhiri na mwenyekiti wa kamati ya safari za nyanjani na Daktari Mjuba; Mhadhiri na mwenyekiti wa kamati ya shahada za juu idarani. Wote hawa ni wahadhiri wanaoendeleza uhasama na maovu chini ya kiongozi wao ambaye ni mwenyekiti wa idara. Uhasama huo ni kama vile kukubaliana na kutekeleza kikasuku Mawazo ya bosi wao liwe liwalo, ukandamizaji wa wanafunzi walioko kwenye usimamizi wa mrengo wa wapinzani wao pamoja na vitendo vingine vya kiufisadi idarani. Ni

kutokana na mielekeo yao dhalimu ambapo safari ya kimasomo ya wazamilifu inakumbwa na hali ya ati na kujaa utata na utelezi. Kupitia kwa wahusika hawa\, tunawaona kwa kuwasikia wahusika wengine chuoni ambao ni wakuu wa chuo ambao nao tunahisi wamechangia kujiwekea vibaraka na vibarakala humo chuoni ili kuendeleza udhalimu kwa manufaa yao ya kibinafsi.

Taswira inayoakisiwa na tamthilia hii ni ya changamoto si haba kwa wasomi hao. Kwenye jalada, mtunzi anaeleza ndoto na matamanio ya wasomi hao wa kiwango cha juu. Anadai wasomi hao huwa na mkikimkiki na ilihamu ya kufanikiwa kwa kusoma na kusonga mbele kitaaluma. Ndoto hizo huzizima na kuzima ghafla kama mshumaa uliotumbukizwa majini. Hili hutokana na changamoto nyingi wanazokumbana nazo wasomi hao wazamilifu. Mtunzi kupitia wahusika Mahiri na Mwanamkiwa anatumia taswira ya mashua iliyo kwenye bahari inayokumbwa na dhoruba pande zote kiasi cha kutaka kuzama baharini. Japo wasomi hao wana bidii ya mchwa wanaojenga kasri kwa mate, na matumaini makubwa sana ya kufanikiwa kitaaluma kimstakabali, wanatingwa kulia kushoto na mawimbi na dhoruba za mazingira ya chuoni kiasi cha kuhisi kusakama na kutamauka.

## 1.2. Kuhusu Mtunzi

Gakuo Joseph Kariuki ni Mhadhiri Mwandamizi wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Bomet. Amebobea katika uwanja wa fasihi ya Kiswahili na mawasiliano. Amesomea shahada ya ualimu (B'ED Arts-1989) na shahada ya Uzamili (M'Phil- 1993) katika Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Moi. Ana shahada ya Uzamifu katika Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta (2014). Isitoshe, amewahi kufunza Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya kwa takriban miaka ishirini alikohudumu hadi kufikia kuwa Mwalimu mkuu wa Shule ya Upili kabla ya kujiunga rasmi na Chuo Kikuu cha Kenyatta mnamo mwaka wa 2010 alikofundisha kwa miaka kumi kama mhadhiri wa Kiswahili kisha kujiunga na Chuo Kikuu cha Bomet. Amewahi pia kuwa mhadhiri wa taaluma ya Kiswahili nchini Uganda katika Chuo Kikuu cha Kikristo cha Uganda (UCU) mjini Mbale kwa muda wa zaidi ya miaka mitano kuanzia mwaka wa 2005.

Amefanya kazi ya usimamizi na utahini wa Kiswahili na fasihi ya Kiswahili kwa muda mrefu katika viwango mbalimbali. Amewahi pia kushiriki katika kuandaa mtalaa na mafunzo ya Kiswahili na fasihi ya Kiswahili katika taasisi mbalimbali nchini Kenya ikiwemo K.I.E. Amewahi vilevile, kuwa mshauri na mwandalizi mkuu wa mtalaa wa Kiswahili kwa shule za sekondari nchini Sudan Kusini miongoni mwa shughuli zingine. Dakt. Gakuo ni mtunzi na mwandishi wa Makala mengi ya Kiswahili. Kadhalika ameandika hadithi fupi nyingi za Kiswahili, Novela, Tamthilia na Riwaya kama vile Safari ya Nyanjani, Ubabe, Safari ya Makerere mtawalia miongoni mwa zingine. Kwa sasa anafunza Kiswahili (fasihi na mawasiliano) kama mhadhiri mwandamizi katika idara ya Sanaa, Utawala na Taaluma za Mawasiliano katika chuo kikuu kishirikishi cha Bomet.

## 1.3 Usawiri wa Changamoto Zinazokumba Wazamilifu

Katika sehemu hii tunashughulikia kiini cha makala yetu ambacho ni usawiri wa changamoto zinazokumba wazamilifu katika tamthilia ya *Ubabe*. Changamoto hizi kwa mujibu wa mtunzi ni nyingi zingine zikiwa kubwa kiasi cha kutinga masomo ya wazamilifu hao. Zingine ni za kibinafsi ilihali nyingi zinatokana na mazingira ya chuoni wanamosomea. Nyingi ya changamoto hizi zinadhihirika katika sehemu ya utangulizi ya tamthilia, onyesho la tatu, na kuendelea.

### 1.3..1 Athari za Vita vya Kiubabe Miongoni mwa Wakufunzi

Wazamilifu wanajikuta katika njia panda wanapogeuka nyasi baina ya fahali wawili wapiganapo idarani. Hili linawapelekea kutamauka kabisa kinyume na shamrashamra walizokuwa nazo wakati wakijiunga na uzamilifu. Wanashangaa kuogundua kwamba walilolipapia na kulitamania halikuwa rahisi kulipata. Patashika na kinyang'anyiro cha ukuu baina ya mirengo miwili inayozozana ya wakufunzi idarani kinawageuza waathiriwa wa vita hiyo. Haya yanadhihirika pale mwanzoni mwa tamthilia tunapomkuta Mahiri na Mwanamkiwa wakiwa kwenye kibarua cha ufunzaji wa muda wanapolalamikia hatima zao baada ya kulambishwa sakafu kimakusudi na Mbabe na jeshi lake. Mathalan, wanasema:

MAHIRI: Vipi kigogo? ***(akimsabahi Mwanamkiwa)***

MWANAMKIWA: Salama Mhenga. **(akiitikia kwa madaha na mzaha)** Mbona uniite kigogo na huku ukijua fika mambo yalivyoniendea visivyo?

MAHIRI: Usijali kuinamako ndiko kuinukako eti, na wimbo mui hauombolezewi mwana! Hata mimi unajua naitwa Mhenga huku uhenga wenyewe nikiwa mbali nao.

MWANAMKIWA: Je ushapoa mori kwani siku nyingi nimekuona ukijipurukusha na kutebwereka huku umejiinamia kama kobe mtunga sheria?

MAHIRI: Imebidi nijitie nguvu kwani masomo yamekuwa kama mtu anayeabiria mashua kuvuka bahari pana. Wajua tena bahari ni uwanja wa fujo.

MWANAMKIWA: Ikiwa bahari ni uwanja wa fujo basi umahiri na uzamifu ni uwanja wa foliti. Tangia niache kufundisha eti nizamie lulu ya masomo ya shahada ya juu, nimejikuta nikizama ima fa ima baharini nisipate mkombozi!

MAHIRI: Walisemaje kuhusu suala lako la utafiti?

MWANAMKIWA: Wacha tu. Niliona giza na nyota vyote mchana! Ilikuwa siku ndefu sana. Ilisemekana kuwa suala lenyewe halikuwa na fokasi, na pia eti nadharia haikujitokeza! Utafiti unaoelekea kuwa sawa na huo, ilidaiwa kwamba uliwahi kufanyika katika idara jirani. Nadharia iyo hiyo nijuavyo mimi, iliwahi tumika katika kuelekeza uzoaji data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji matokeo. Nilijikakamua lakini wapi! Je na kuhusu utafiti wako?

MAHIRI: Suala langu lilipingwa kwa dhati. Pamoja na kuwa lilikuwa likieleweka barabara na nadharia kuwa wazi, ilidaiwa kuwa mada imechakaa. Kwa hiyo, ilinilazimu kuibua suala lingine jipya la utafiti. Fikiria ilikuwa ni baada ya kuidhinishwa kwa makala dhanishi na si wengine, bali wanaidara hao hao. Mbona wakangoja hadi siku ya utetezi kunibwaga sakafuni tena kwa nguvu na vibaya vibaya? Lo makubwa hayo! Nilibaki sakafuni kinywa wazi tena nikiwa nimetamauka. Nilihisi kama mtu aliyekumbana na kirimbi shingoni mwake.

MWANAMKIWA: Na wasimamizi wako hatimaye walisemaje?

MAHIRI: Lipi lingine tena, ila eti nizingatie ushauri wa kikao cha idara! Hata hivyo, nilihisi Profesa Mbasi alikuwa amefadhaika na kuwa mwenye hisimseto. Alinipa moyo kwamba ningefanikiwa hatimaye, ila nihifadhi kumbukumbu za kikao kwa matumizi ya halafu… Alinishauri kuibua suala la utafiti katika eneo la ushairi ambalo nadhani amebobea

kwalo. Alinipa nakala kadha za majarida na Diwani za watunzi mbalimbali wa ushairi kudurusu. Alinishauri kuwasiliana naye wakati wowote nilipofikiria kuhusu suala muafaka.
Hapa inadhihirika wazi kwamba hawakufeli ila ilibidi wafelishwe kukidhi matakwa ya mrengo wa Mbabe. Hatimaye, kwenye tamthilia inagundulika kwamba ilibidi uamuzi huu kufanywa kwa njia ya upigaji kura. Mirengo yote miwili ipata idadi sawa ya kura. Hili lilimpelekea mwenyekiti wa idara kupiga kura yake kutoa uamuzi wa mwisho. Ajabu ni kuwa mwenyekiti huyo bila ya kujali wala kubali, alipiga kura yake ili kuafikiana na mrengo wake uliotaka kuwafeli wazamilifu. Hili likawa na matokeo ya aina moja tu; kwamba wazamilifu wote waliotetea mapendekezo yao katika kikao hicho walifeli. Katika ukrasa wa 7, Mahiri anazungumzia kuhusu vita hivyo vya kiubabe miongoni mwa wakufunzi hao:

MAHIRI: Uongozi bwana! Uongozi ni serikali. Serikali ni siri kali. Sera za kila kiongozi ni dhahiri kwa matendo yake. Isitoshe, kuna kidumbwedumbwe. Ni kama vita vya mafahali wawili. Wewe huoni hivyo? Mwenye macho haambiwi tazama! Kila idara pale chuoni ina hujuma zake kwa sisi kina yahe. Kuna pia mirengo ya kulia na kushoto miongoni mwa wahadhiri. Mashambulizi na migogoro inapotokea baina ya makundi hayo, hasa kuhusu mielekeo na falsafa zao tofauti tofauti, basi nyasi ndizo huumia. Itokeapo hivyo mwendo wetu wa kimasomo hugeuka na kuwa kama wa hombwe badala ya mambo kwenda kikakakaka. Wewe unadhani ni nini kiini cha kamba ya mvutano miongoni mwa wanataaluma hao inayotufanya kutaahari kimasomo?

MWANAMKIWA: Sababu ni nyingi. Kuna hicho kinachodaiwa kuwa PhD yaani P-H-D

MAHIRI: Najua wengine wamesema kwa mzaha eti PhD ina maana “Pengine Hana Digrii”.

MWANAMKIWA: Siyo hiyo tu, inadaiwa kuwa PhD ni asili ya wehu yaani kichaa kikali. Mtu anasoma mpaka akili zake zinageuka kiruu!

MAHIRI: (***akikubali kwa ishara ya kichwa)*** Naam, ‘Permanent Head Damage’. Hili linashadidiwa na wanasaikolojia wanaotukuza nadharia kwamba kila mwanadamu ana asilimia kiasi cha wehu. Ni kiwango cha wehu ndicho kinachopitilizana baina ya wanadamu. Wengine wakawa wamekoleza na kukolea zaidi katika wenda wazimu huo, wengine wakawa na kiasi tu.

MWANAMKIWA: Hivi huenda hata kile tunachodhania kuwa hekima na maarifa kikawa ni stihizai na sarakasi tu?

MAHIRI: Kama ni sarakasi basi hiyo ni sarakasi ya kipekee kwani pia ina manufaa yake na inatambulika kote duniani. Humfanya mja kuwa mshonde kwa waja wenzake.

MWANAMKIWA: Nadhani pia hio sarakasi imetamalaki chuoni hadi kileleni kwani imekita mizizi. Hii ndio huenda ikawa kiini cha mambo aghalabu borongo borongo.
MAHIRI: Ndio, pwagu hupata pwaguzi. Hata utawala wa chuo nasikia hupendelea sarakasi hiyo ili kuendelea kutesa. Fikiria mwenyekiti mzima asiyejali sana wateja wa chuo ambao ni wanafunzi na hatimaye wakufunzi.

MWANAMKIWA: Mbona chuo kisiwe na sera maalum ya uteuzi wa viongozi wake wa idara na vitivo mbalimbali au hasa kitoe mafunzo faafu kwa wakufunzi yanayohusiana na utawala?

Kutokana na dondoo hili, inabainika kwamba vita sugu baina ya wakufunzi ni donda ndugu ambalo limekita mzizi vyuoni. Hali hiyo inapatikana katika vitengo vingine vya utawala wa vyuo vikuu kiasi cha kuendeleza ufisadi unaodumaza.

### 1.3..2 Kubwagwa na Kufelishwa Visivyo

Kufelishwa visivyo huko kuliwapelekea na kuliwapa jakamoyo wazamilifu hao. Wengine walichanganyikiwa kabisa wasijue ni kwa nini wakajitoma kwenye masomo hayo ya juu. Walitamauka na kupoteza ari waliokuwa nayo mwanzoni. Ndoto zao za kujikwamua na kujiendeleza kiakademia na kimaisha zilizima ghafla. Sababu za kufeli huko si kwamba walifaa kunoa, bali ni kwa sababu wanasimamiwa na wakufunzi wasiounga mkono mrengu wa mwenyekiti.Mapendekezo yao licha ya kuwa mazuri yanasemekana hayafai kwa sababu nyingi zisizoeleweka za kusingiziwa; (kwamba mada haina fokasi, mada imechakaa, nadharia haijitokezi vyema, utafiti sawa na huo umewahi kufanyika..nk)

Ilibidi kukakawana na kuwaza na kuwazua tena ili kufikiria kwenda mbele tena. Hili ndilo tunaloliona kati ya mahiri na Mwanamkiwa wanapopiga moyo konde na kusema:

MWANAMKIWA: Unaonaje bwana mkuu? Je, haifai tujikakamue na kufanya maazimio mapya?

MAHIRI: ***(akiitikia kwa kichwa)*** Ni kweli kabisa. Itabidi tupoteze kitu kimoja badala ya vyote viwili kwani, mwangata mbili moja humponya. Naona turejee chuoni tena bila kujali wala kubali. Turejee tena kwa kishindo. Turejelee maoni ya walimu wetu wazuri na wema. Turejelee mawazo yao na yale ya idara na kupiga hatua tena kwa moyo wa kutokata tamaa wala matumaini.

MWANAMKIWA: Nakubaliana nawe mia kwa mia. Jana usiku niliota ndoto. Ilikuwa ni ndoto ya ajabu na ya matumaini. Niliota mimi na wewe tunakwea mlima mrefu sana tena uliokuwa wima kabisa. Tulianza kama mchezo huku tukikurupuka kwa madaha na mikogo kama wafanyavyo Watoto wanapocheza na kushindana mbele ya halaiki ya watazamaji. Tuliuparamia na kuukwea kwa pupa na kwa arubii. Shina lake ulikuwa kabambe nchani ulikuwa kabibu. Tukauparakasa. Kutanabahi, tunajikuta karibu na kilele. Tulipojaribu kutazama huko chini tulikoanza safari ya ukwezi, tuliona kioja. Kulikuwa mbali sana na isitoshe, mteremko ulikuwa mkali kiasi hatungeweza kurejea huko salama kwa vyovyote vile. Mara tulishikwa na hofu kubwa ya maangamizi na kujutia kuanza ukwezi wenyewe. Afua ikasalia moja tu, kukwea tu zaidi liwe liwalo. Tulipiga moyo konde na kuamua kujizatiti kuendelea. Tulichechemea na kwa uwezo wa nguzu zetu zote, tukachuchumia kileleni. Ajabu ni kwamba tulipofikia kilele cha mlima huo, tulishangaa kuona sehemu tambarare iliyoelekea na kupakana na baraste iliyokuwa na magari na wapita njia wengine. Tulichapua miguu na kuparakasa kuifikia barabara hiyo kuu. Gurufu yenyewe ilikuwa imesakifiwa vyema huku ikiwa na safu nne za magari kila upande; kulia kushoto. Mara nilizinduka kutoka usingizini na kujikuta napaparika kitandani huku mwili mzima umelowa kwa jasho.

MAHIRI: Ndoto kali sana hiyo. Kukwea daima ni kiashiria cha mafanikio maishani. Mlima mrefu uliochonga kwangu naona ni kiakisi cha safari yetu ndefu ya usomi iliyojaa vizuizi, changamoto elfu elfu na utelezi si haba.

**1.3..3 Kucheleweshwa Kufuzu**

Kutokana na kindumbwedumbwe cha ubabe, safari ya masomo kwa wazamilifu hao inakuwa ndefu kupindukia. Wanachukuwa muda mrefu kukamilisha shahada ambazo kwa kawaida zilifaa kuchukuwa muda mfupi wa miaka miwili au mitatu kwa uzamili na uzamifu mtawalia. Hili linawapelekea wengi wao kukengeuka kwa kukosa kutimiza malengo na muda wa masomo yao ya juu. Kilele chake ni kudidimia kwa matumaini. Hali hii inadhihirika pia katika onyesho la tatu katika kigwena cha mwenyekiti wa idara. Inashuhudiwa kwamba jeshi la Mbabe liliathiri masomo idarani kwa kutumia hila na ucheleweshaji:

MBABE: Mwambi kweli kweli kwa mambo ya wengine! Unaweza hata kutuzwa tuzo la shujaa wa uhinivu ***(anacheka kwa kejeli)*** Hata hivyo, kwa kweli sote tulionja asali ila twahitaji zaidi. ***(akijichekea kijingajinga)*** Na wewe Mjuba, leta uhondo wa kamati ya kiakademia!

MJUBA: Bwana Mkuu, asante kwa kuniunga mkono na kwa ushauri kila nilipokujia. Kwa hakika mambo yalienda kama tulivyokusudia. Tuliitumia kamati hii kama uwanja wa vita. Kwayo, tuliwafyeka mahasidi na tukabaki wenye kusema humu idarani. Tuliwachunguza na kuwachuja maadui hasa wenye viherehere na kuzamisha majahazi na mashua ya wanafunzi wao baharini vibaya vibaya.

MBABE: Pasua mbarika tujuwe ni melikebu ngapi zilizozamishwa na manowari yetu.

MJUBA: Ni merikebu zote, zilizodhubutu kupeperusha beramu za mahasidi wako. Za mwisho mbili zilikuwa za Mahiri yule mzamifu na ya yule Bibi akiitwa nani vile?

MBABE: Mwanamkiwa.

MJUBA: Naam, huyo huyo Mwanamkiwa aliyetaka kujifanya Mekatili wa Menza katika darasa la shahada ya juu eti kwa sababu kashauriwa na wakwasi wa taaluma! Tulifanya juu chini kuharamisha tafiti zote zilizopewa kipaumbele na wapinzani wetu. Tulitumia mbinu elfu elfu kufanikisha hili. Mara tulidai utafiti kama huo unaendelea sijui Pwani au eneo la Ziwani, mara mada imechakaa, mara mada haikuwa na fokasi, mara nadharia haikujitokeza, mara utafiti haukuwa na mchango wowote wa kiakademia, mara mada haikukaakaa vizuri, mara mada ilikuwa finyu, mara data ya uchunguzi haingetosha kiwango cha utafiti na kadhalika na kadhalika. Waathiriwa walishauriwa kuibua mada nyingine kana kwamba uibushaji wa mada ulikuwa tendo la kurejea dukani na kununua upya bidhaa nyingine! Mrengu wa kushoto ukawa umechoka. Wengine walilalama. Wengine wakaudhika sana. Baadhi walianza kujiondoa kwa usimamizi wa wanafunzi ilihali, baadhi walisikika wakiwashauri wanafunzi kutafuta muelekeo kutoka kwenye ufalme, himaya na ngome yetu. Si hayo tu, baadhi ya wanafuu walitamauka na kuinua mikono. Kuna wale inadaiwa walisikika wakitoa kauli mbiu kuwa ‘bora uhai’ kutokana na kufadhaika kwao. Mchezo si mchezo? Safari ya kiakademia ikafanyika tata, telezi na yenye ugiligili, na wala si kama hasidi mmoja alivyosikika akidai eti ‘someni kwa furaha’.

MBABE: Shukrani Mjuba kwa ujuba na kwa kazi nzuri hasa kuhusu hilo la kuwakomesha na kuwatokomeza wapinzani wetu. Wewe ndiye mjuba wa wajuba wote. Ingelikuwa ni mimi, nigefanya vivyo hivyo au hata zaidi kukabiliana na maadui. Vita havina macho na wapiganapo fahari wawili, nyasi huwa hazina budi kuparurika pamoja na ardhi inazozihimili. Ila kuna tatizo. ***(Kimya)*** Kazi yako imeelekea kututia matatani.

Mwenyekita kupitia kwa mshirikishi wa shahada za juu amegeuza uzamilifu kuwa uwanja wa vita. Lengo lake ni kudhihirisha kwamba yeye na mrengu wake ndio wenye kusema pale idarani. Hali inakuwa si hali tena kwa wazamilifu hasa wanosimamiwa na na mrengo wa pili. Mambo yanakuwa kinyume mbele kwani idara inapaswa kuwasaidia wasomi wake kupiga hatua badala yake idara inawatinga wasomi hao.

### 1.3.4 Mgogoro Baina yao na Waajiri Wao

Muda mrefu kimasomo kuliko mkataba wa livu ya masomo waliopewa unaibua changamoto kubwa. Muda wa livu unamalizika ilihali masomo yenyewe hayajafika hata katikati. Wanaelekea kuchukuliwa waongo kwani livu zinakamilika pasina wao kuwa wamerejea kazini. Hili linawapelekea kukaribia kukosa vyote (si masomo si kazi). Hili ndilo linalowapekea kina Mahiri kusema:

MWANAMKIWA: Mimi nimeacha na kusitiza kazi yangu ya serikali, nikaasi hata na ndoa yangu, na sababu, sababu yake nini? Eti nachuchumia shahada ashirafu ya juu zaidi ili inizidishie tonge na kunibadilishia mchuzi; badala ya sima na maharagwe, nipate wali na mchuzi wa kuku wapi? Nimekuja kujutia mwenyewe, nilichokitazamia sicho ninachoelekea kukipata! Naelekea kutamauka kabisa na kukumbwa na huzuni juu ya kupoteza muda wangu bure. Naelekea kukosa mahali pa kuficha uso wangu kwa haya, majuto na tahayuri.

MAHIRI: Pole sana dadangu. Nakuelewa jinsi ulivyokumbwa na mhashara hadi ukalazwa gangoni kutibiwa. Hata mimi niliomba livu, nikaacha kazi na kuipuuzilia mbali aila yangu. Nakumbuka mtoto wangu mdogo wa kike Joy aliyemzoelea babake alivyolia nilipowaaga yeye na mamake kuja chuoni kuzamia eti taaluma. Alilia na kupaparika ungedhani malaika yule kanionea jinamizi na jini likinitambalia nisijue wala kuliona mwenyewe. Hata sasa nafika nyumbani mara moja moja na mke naye… uk 12.

Mjadala huu baina ya wawili hawa unaakisi changamoto hii ya kucheleweshwa kukamilisha masomo. Athari zake ni nyingi ikiwemo kusongwa kwa mawazo kiasi cha kulazwa hosipitalini. Isitoshe, wanapatwa na kimako cha ni nini watakachowaeleza aila na marafiki wao endapo wakose kufaulu kimasomo. Kadhalika, wamepatwa na tahayuri wasijue pa kuficha nyuso zao. Masomo yanageuka karaha badala ya kuwaletea raha.

### 1.3.5 Mgogoro Baina Yao na Aila Zao

Kuchelewa kuyatimiza malengo yao ya elimu kunawaweka kwenye njia panda kifamilia. Kwendea masomo hayo ya juu ni sawa na kupuzilia aila zao. Hili ndilo linalompelekea Mahiri kukumbukia kwa huzuni jinsi bintiye mkembe Joy, alivyolialia alipomuaga yeye na mamake kwenda masomoni. Hali sawa na hiyo imeshuhudiwa miongoni mwa wazamilifu wote. Ilibidi wote hao kupuuzilia familia zao (wake/waume na watoto), japo kwa muda.Wanyumba wanaelekea kuwashuku kutokana na kigezo cha muda wanaotumia kinyume na matarajio. Hili nalo linaelekea kuwatia aibu (kukosa la kuwaambia wanyumba, wanaonekana kuwa wapumbavu waliolemewa kimasomo au hasa wajanja). Mathalan Mahiri katika ukurasa wa 13, anakiri:

*Journal of African Interdisciplinary Studies (JAIS)*: **ISSN 2523-6725** (online)
**October 2024 Vol. 8, No. 10**
**Citation**: Jeptanui, S & Gakuo, J. K. (2024). Usawiri Wa Changamoto Zinazowakumba Wazamilifu Katika *Ubabe. Journal of African Interdisciplinary Studies*, 8(10), 405 – 420.

MAHIRI: Pole sana dadangu. Nakuelewa jinsi ulivyokumbwa na mhashara hadi ukalazwa gangoni kutibiwa. Hata mimi niliomba livu, nikaacha kazi na kuipuuzilia mbali aila yangu. Nakumbuka mtoto wangu mdogo wa kike Joy aliyemzoelea babake alivyolia nilipowaaga yeye na mamake kuja chuoni kuzamia eti taaluma. Alilia na kupaparika ungedhani malaika yule kanionea jinamizi na jini likinitambalia nisijue wala kuliona mwenyewe. Hata sasa nafika nyumbani mara moja moja na mke naye…

MWANAMKIWA: ***(anamkatiza na kudakiza)*** Mke ameanza kukushuku mapenzi umeyatia maji pengine hata una wa kando…

MAHIRI: Siyo hiyo tu, anauliza kwani shahada ya miaka mitatu imegeuka na kuwa ya miaka mitano? Kwake mwezi mmoja ni sawa na mwaka! Nashindwa kumweleza kwamba nimesakama. Wakati mwingine hutaka kumpasulia mbarika lakini nikajizuia kwa kuchelea

MWANAMKIWA: Najua unachelea kujiumbua mwanamume wewe wa Kiafrika. Ubabe dume utawamaliza nyinyi kaka zetu. Au unachelea mke atachapuka na kuchungulia nje kwa kuzidiwa na mihemko na jazba!

MAHIRI: Si vile hasa, ila wenye haya wana mji wao. Wajua tena ada ya mja ishanena muugwana ni kitendo na kwamba, subira yavuta kheri. Leo mimi na wewe tumesadifu kujikuta humu tukifanya kibarua huku siku za livu zetu zikiyoyoma. Karibuni tutapata barua na ilani za kurejea kazini. Mara tutajikuta kwenye njia panda tusijue kuinua mikono kuhusu masomo na kurejelea amali zetu, au tuinue mikono kuhusu kazi na kurejelea masomo liwe liwalo. Kwa vyovyote vile, kuna gharama inayohitaji uhasibu tena wa hali ya juu!

Mahiri anadhihirisha kuwa wazamilifu wamo katika njia panda hivi kwamba "tusijue kuinua mikono kuhusu masomo na kurejelea amali zetu, au tuinue mikono kuhusu kazi na kurejelea masomo liwe liwalo…' Yote hayosi kutokana na kulemewa kutokana na kushindwa kimasomo. Ni kutokana na uhasama uliopo idarani kwa wazamilifu hao kutokana na vita vya kiubabe.

### 1.3..6 Msongo wa Mawazo

Pilka pilka za kimvutano zinawapekea wengi wa wasomi hawa kupatwa na ugonjwa wa mawazo. Ugonjwa huo unatokana na Mhashara ambao nao unasababishwa na kuwaza na kuwazua kupindukia.Wengine wao kama Mwanamkiwa, wanalazwa hospitalini na kuwa katika hali mbaya kiafya. Isitoshe hili linaibua majuto ya kuchelea kuanza wasichoweza kumaliza! Hili ndilo analolidokeza Mahiri anapomliwaza Bi Mwanamkiwa kwa kusema:

MAHIRI: Pole sana dadangu. Nakuelewa jinsi ulivyokumbwa na mhashara hadi ukalazwa gangoni kutibiwa. Hata mimi niliomba livu, nikaacha kazi na kuipuuzilia mbali aila yangu. Nakumbuka mtoto wangu mdogo wa kike Joy aliyemzoelea babake alivyolia nilipowaaga yeye na mamake kuja chuoni kuzamia eti taaluma. Alilia na kupaparika ungedhani malaika yule kanionea jinamizi na jini likinitambalia nisijue wala kuliona mwenyewe. Hata sasa nafika nyumbani mara moja moja na mke naye…

MWANAMKIWA: ***(anamkatiza na kudakiza)*** Mke ameanza kukushuku mapenzi umeyatia maji pengine hata una wa kando…

MAHIRI: Siyo hiyo tu, anauliza kwani shahada ya miaka mitatu imegeuka na kuwa ya miaka mitano? Kwake mwezi mmoja ni sawa na mwaka! Nashindwa kumweleza kwamba nimesakama. Wakati mwingine hutaka kumpasulia mbarika lakini nikajizuia kwa kuchelea uk 12

Hapa, Mwanamkiwa anakuwa kielelezo tu cha madhara ya afya kutokana na msongo wa mawazo yanayowakumba wazamilifu chuoni. Wengi wa wazamilifu hao wanaelekea kupatwa na matatizo ya kiakili kutokana na kulemewa au kulemazwa kimasomo. Hali inakuwa tete na telezi kama mtunzi anavyokiri katika baadhi ya kazi zake. Mahiri na Mwanamkiwa wametumiwa kama wahusika watunzi wanaoakisi msimamo na falsafa ya mtunzi huyu. Ni dhahiri kwamba mtunzi kakereka si kidogo kutokana na mambo yanavyokwenda katika taasisi ya masomo ya juu. Kwa maoni yake, wanafunzi wanafaa kusoma kwa furaha na kufuzu kwa muda uliotengewa shahada husika. Haiyumkiniki ni vipi na ni kwa nini vyuo vikuu vikageuzwa uwanja wa vita miongoni mwa wenye nguvu na hivyo kuwabughudhi na kuwatinga wateja wa vyuo hivyo ambao ni wanafunzi wasiokuwa na hatia. Isitoshe, wateja hao wameshalipia kikamilifu karo za masomo hayo. Inapotokea kwamba wamejikuta katika kinyang'anyiro hicho cha vita, wanashindwa wafanye nini ili kujikusuru na jinamizi linalowakabili.

### 1.3.7 Kujikuta Njia Panda

Wazamilifu wanajipata wamechanganyikiwa na kuwa katika hali ya switafahamu. Bidiii walizokuwa nazo mwanzoni zinayeyuka na kuwaacha wakishangaa na kujihurumia. Wanagundua kwamba walichokienzi, kukitamani na kukitaka tokea mwanzo hawakukijua vyema. Ilikuwa ni kama kujipalia makaa ya moto na kukimbiza tufani. Wanapotanabahi, wengi wao wanachukia uzamilifu, wanajichukia na kuchukiwa kila kinachoendana na masomo haya si wakufunzi, si idara si utawala wa chuo, si sheria za chuo si nini. Hili ndilo linalomfanya Mahiri na Mwanamkiwa kukiri:

MWANAMKIWA: Sheria, sheria za huku Uafrika zimewekwa kumhujumu mnyonge na kumtetea mwenye nguvu. Visa kama hivyo vimezidi kuogezeka vyuoni. Wanafunzi wajanja wameamua kutumia ugiligili uliopo wa sheria za kukabiliana na shutuma za nyanyasa mapenzi kuwachimbia walimu wao. Aibu iliyoje? Na watawala nao ni kama wenye njaa ya kadhia za namna hiyo! Hayo ni matumizi mabaya ya mamlaka. Ona sasa tulivyowekewa sheria za kutuangamiza kabisa, ilihali sisi tumejikakamua na kutenda lililobidi ila tukachezwa shere! Mkoloni bwana hakuenda, alibadilisha tu umbo. Ukoloni ungalipo hata kwenye taasisi na vyombo vya nchi. Ni ukoloni huo unaovuruga mambo ya elimu idarani.

MAHIRI: Isitoshe, cha mno pia ni ubabe. Ni sawa na tunayoyashuhudia kila uchao katika ulingo wa siasa. Kila kiongozi anajizatiti kutangaza mrengo wake wa siasa. Timu zao nazo zimepewa majina ya ajabu ajabu; 'Tanga Tanga', 'Kieleweke', 'Handishake', 'wiper', 'mashinani', 'azimio', 'Kenya Kwanza' na kadhalika. Kila mmoja hutaka kudhihirisha yeye ndiye mwenye kusema kuanzia siasani hadi utawalani. Vyuoni kuna kukurukakara za ushindani. Kila mhadhiri hutaka kudhihirisha kwamba yeye binafsi ndiye aliyebobea kuwazidi wenzake. Maisha ni kinyang'anyiro eti. Ni enzi ya 'kuwajua watu' kama ilivyodaiwa na mkuu mmoja Kenya! Hujaona wanavyojitapa darasani?

MWANAMKIWA: Eh tena sana ***(akiigiza)*** 'mimi nimesomea na kuchapa kazi ughaibuni…kule ng'ambo ulimwengu wa kwanza…asili na kitivo cha maendeleo ya ulimwengu. Umemsikia nani mtu kama mimi humu chuoni? Shahada yangu ya uzamili ni

*Journal of African Interdisciplinary Studies (JAIS)***: ISSN 2523-6725** (online)
**October 2024 Vol. 8, No. 10**
**Citation**: Jeptanui, S & Gakuo, J. K. (2024). Usawiri Wa Changamoto Zinazowakumba Wazamilifu Katika *Ubabe. Journal of African Interdisciplinary Studies,* 8(10), 405 – 420.

nzito kuliko ya uzamifu kutoka ulimwengu wa tatu. Nikiongea kuhusu uzamifu, nastahili kuwa kwenye utingo hasa wa chombo cha chuo hiki! Hiyo ni shahada ya kupata wala si ya kupewa kama hizi zinazoringiwa humu Afrika. Hata hayo mashangingi yangu sijui mangapi vile, nimeyanunua kwa madola kutoka maduka ya magari katika ulimwengu wa kwanza. Si mauzo ya mitumba kutoka ughaibuni kama hayo yanayoendeshwa na wengine chuoni humu ha!'

MAHIRI: ***(anacheka kwa kuathirika na maigizo na maneno ya Mwanamkiwa)*** Hivi wewe binafsi ukiwa mhadhiri na profesa mwanandamizi idarani humu utafanyaje?

MWANAMKIWA: Wala usiniulize. Huo utakuwa wakati wangu wa kujisheua na kujitanua! Utakuwa wakati wangu kujua kilichonikengeusha na kunisagasaga miaka mingi. Aisee! Nakuapia kila mwanafunzi wangu atajua nilivyoteseka kufikia kiwango hicho cha ufanisi. Nitalipiza tu kisasi mimi! Taamali hilo. (***anashangaa kumuona mwenzake alivyomkazia uso na kumtazama kwa jicho la bezo) uk 11***

Dondoo hili linadhihirisha athari ya vita vya kiubabe kwa wazamilifu. Wanaulinganisha udhalimu wanaopitia na ukoloni mamboleo. Hii ndio inayomfanya mwanamkiwa kuungama kwamba mkoloni hakung'atuka eti kwamba alijibadilisha tu sura. Wanaona udhalimu huu kama matumizi mabaya ya mamlaka ambayo yanaelekea kumuangamiza mnyonge asiyekuwa na haki. Wanalinganisha kinyang'anyiro hiki na hali ya vuta nikuvute ya siasa nchini Kenya ambapo wanasiasa inadaiwa huraruana bila huruma. Pamoja na hayo, wanalinganisha uozo huu na ubaguzi, kudhuluma kwa wanyonge na wasiokuwa na hatia. Wanazungumzia majitapo ya wahadhiri kama si kitu cha kufaharikia ila cha kuaibisha. Kwa upande mmoja tunaona athari hasi ya kimstakabali ya hayo kwa baadhi ya wazamilifu. Mwanamkiwa anatamani pia kupata nafasi ya kujilipizia kisasi endapo atabahatika kuwa profesa katika chuo kikuu. Inamlazimu Mahiri kumkemea na kumwambia haifai binadamu kulipiza kisasi.

### 1.3.8 Wasiwasi Hofu na Woga

Hali tete ya kimasomo inawafanya wazamilifu kupatwa na wasiwasi. Hili linawanyima furaha ya kuendelea na maisha ya kila siku. Japo tunawaona wakitia bidii ya hali ya juu kimasomo tunawaona wakiwa na hofu ya huenda wasifue dafu masomoni hayo. Wazamilifu wanadhihirisha ujasiri na uelewa masomo kupitia darasa la Profesa Mzee wanapowasilisha hoja faafu walizozitafitia kuhusu mawazo ya Plato kuhusu ushairi. Hadhira ya wasomaji wanagundua kuwa licha ya Profesa Mzee kuwa mahiri katika ufundishaji, wanafunzi wake wanaelekea kuwa kama yeye kutokana na juhudi wazozitia masomoni.

Kadhalika, tunawaona wakifanya mwigo wa mawasilisho ya mapendekezo yao. Kipindi hicho kinadhihirisha kwamba baadhi ya wazamifu hao akiwemo Mahiri, Mwanamkiwa na Bi Maridhia kwa kuwataja tu wachache wamebobea katika masomo ya shahada za juu. Baadhi hata wako tayari kuchukuwa nafasi za ukufunzi vyuoni endapo wanaweza kupewa fursa hiyo. Isitoshe, kupitia vikao vya wahadhiri kikiwemo kigwena cha mwenyekiti, tunagundua kwamba Mahiri alikwangura alama ya A katika kila kozi aliyofunzwa chuoni. Mwanamkiwa naye alipata A katika karibu kozi zote isipokuwa chache mno alizopata B. Hilo na kwa kuwa kashauriwa na mrengo wa Prof Mzee kuhusu utafiti, lilipelekea baadhi ya wakufunzi pinzani kumkejeli kama aliyelelekea kuwa shujaa kama Bi. Mekatilili wa Menza.

Wazamilifu walijua tu njia moja ya kukabiliana na hofu na uoga uliowakumba. Njia hii ni kujitahidi zaidi chambilecho Mhusika Mtiki katika *Shamba la Wanyama*. Hata baada ya

*Journal of African Interdisciplinary Studies (JAIS)*: ISSN 2523-6725 (online)
October 2024 Vol. 8, No. 10
**Citation**: Jeptanui, S & Gakuo, J. K. (2024). Usawiri Wa Changamoto Zinazowakumba Wazamilifu Katika *Ubabe. Journal of African Interdisciplinary Studies*, 8(10), 405 – 420.

kufanya zoezi la wasilisho mwigo na kila mmoja kujizatiti kukabiliana na kikao chenyewe cha utetezi, tunaona wakiwa wachangamfu ila wenye uoga hofu na wasiwasi. Tunaambiwa hivi:

***Maktabani mwa idara. Wazamili na wazamifu wako kwenye shamia. Wanang'ang'ana kupiga nakshi na msasa mapendekezo yao kabla ya kuyawasilisha rasmi katika kikao cha utetezi idarani. Wengi wanaonekana wenye wasiwasi ijapo wanajikaza kuandaa 'Power Point' za mapendekezo yao ya utafiti yanayotarajiwa kuwasilishwa kwenye kikao rasmi cha idara baadaye. Wanafanya kujikumbusha na kukumbushana hatua na masharti maalum na muhimu kuhusu uwasilishaji tarajiwa.***

MAKINI: Ndugu wapenzi wa taaluma ***(akiwaashiria wote ukumbini)*** leo ni siku ya siku. Leo ni siku tukufu. Leo ni leo kwani asemaye kesho ni muongo. Ni siku muhimu na ya kihistoria kwani hata safari ya maili elfu huanza kwa hatua moja. Kwa wote watakaofanikiwa kusonga mbele, daima leo itabaki tarehe ya kumbukizi maishani. Nina furaha kubwa kuwaalika wote kwenye hafla hii ili kila mmoja wetu atufae sote kwa moja au mawili yaliyo muhimu. Pia nina furaha kuwatambulisha wenzetu ambao tumewapeza kwa muda mrefu. Kaka Mahiri na Dada Mwanamkiwa karibuni sana na mjisikie nyumbani. Na kwa kuwa kichwa cha kuku hakihistamili kilemba, naomba mniruhusu kuutwaa wadhifa wa kaimu kiranja wa darasa na kumpisha sogora kamili kutekeleza wajibu wake wa kutuongoza kwa shughuli hii muhimu. Hamna haja ya kuandika kwa mate ilihali wino upo. ***(akimwashiria mahiri)*** Karibu msharafu kiongozi wetu.

MAHIRI: ***(akinyanyuka huku akipigiwa makofi)*** Asante sana kaka Makini. Wahenga hawakukosea walipoamba kuwa mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo, na kwamba kuinamako ndiko kuinukako! Sote tumetoka mbali. Mbali sana huko bahari ya saba kulikojaa mawimbi na vingi vitimbi. Nadhani yote mwafahamu masaibu yaliyonisibu kiasi cha kutamauka na kukata tamaa kabisa kama mnyonge. Mnyonge hana haki. Leo mnanivisha kilemba na kunifanya nihisi hoi kama huyo kuku asiyestahili kilemba kichwani pake. Nilikuwa hata nimesahau kabisa jukumu la ukiranja kwani nilisalimu falsafa kuwa bahari hailindwi. Kabla ya kuendelea, naomba kumkaribisha dadangu Mwanamkiwa (akimwashiria) aseme machache.

MWANAMKIWA: Asante sana Kaka. Kwa kweli kama alivyokwisha kutanguliza ndugu Makini, leo ni siku kuu. Ni siku ya kuzoazoa kila kilichozambaratika na kuvunjikavunjika kama vigae mara elfu. Ukweli ukidhihiri, uongo hujitenga. Sisi kama wanafunzi ni wateja muhimu wa chuo kikuu. Tumelipia ada na karo ya kuwa hapa. Tumejitolea mhanga kwa jino na ukucha kujiendeleza kielimu na hivyo kukiongezea sifa za kitaaluma chuo hiki. Lakini aghalabu tumejikuta katika njia panda hadi tukachanganyikiwa. Tukasahau kabisa haki zetu kama wadau muhimu wa idara na chuo kizima. Tukaishia kudata kati ya migogoro ya watu wengine ambao kimaisha, wameshafika! Tukasahau siri ya nguvu za umoja wetu. Tukasahau sauti ya dhiki ya wanyonge waliosetwa ndio silaha yao! Leo tumeamua kwa kauli moja mimi na kakangu Mahiri kujitoma tena kwenye uga huu wenye utelezi na changamoto si haba. Tunaomba nyote tushikane bega kwa bega tupigane na adui mmoja. Adui huyu ni mtu yeyote atakae kutuponza na kututinga na safari yetu ya kiakademia. ***(akielekeza mikono kwa wanafunzi wenzake kama ishara ya kuwasihi kufanya jambo)*** Je mtakubali tushirikiane? ***(mara wanafunzi wote wanashangilia na kupiga makofi huku wakionyesha ishara ya***

***kidole gumba kama kiakisi cha kuunga mkono hoja iliyotolewa. Anaondoka jukwaani na kumwacha Mahiri kutamba.)***

MAHIRI: Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Tunafaa kuhurumiana na kusaidiana kwani, akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki. Nimekubali kuendelea kuwa kiranja wenu. Tafadhali nitakapowaita pale haja ya kudhihirisha nguvu ya umoja wetu itakapohitajika naomba mjitokeze kwa dhati. Na sasa naomba tuliingilie moja kwa moja suala na ajenda yetu muhimu ya leo kwani wakati una mabawa. Kutufungulia mjadala wa leo, nitamwalika mkuu wetu Mwangwi atushauri na kutupa muelekeo faafu. Uk 17

Hapa inadhirika wazi bidii wanazotia wasomi hawa wa shahada za juu ili kufanikiwa kaika masomo yao. Wanaandaa mawasilisho yao ya 'powerpoint' kama ilivyo ada ya idara. Isitoshe, umoja wao unadhihrika wanapotia shime ya kushikana bega kwa bega kutekeleza kazi hii muhimu. Kiongozi wao wa kikao ambaye ni Makini anadhihirisha waziwazi kwamba huenda baadhi yao wakakosa kufanikiwa katika kikao kinachotarajiwa karibuni, ila kwamba kwa wale ambao wangefanikiwa basi siku hiyo ya maandalizi itageuka na kuwa ya kumbukizi maishani. Ni dhahiri hapa kwamba jitihada haziondoi kudra. Wazamilifu hawa ni kama mtu afumaye pengine gizani kwa kubahatisha tu, huenda asipate au akapata. Tunajua kiini cha kauli mbiu hii ni kwamba mambo hayana budi kuamuliwa na wenye kusema ambao ni Mbabe na jeshi lake. Hayo ndio yanayowapa wasomi hao wasiwasi. Masomo haya yanawaogofya wasijue kama watafaulu japo wasiwasi unawapa kutia bidii zisizo na kifani katika maandalizi, na kukifanya kikao cha utetezi wa mapendekezo kinakuwa kama siku ya kiama.

### 1.3.9 Athari Hasi Kimstakabli

Baadhi ya athari hasi kama tulivyokwisha dokeza hapo juu ni pamoja na wengine kutaka na kuamua kulipiza kisasi. Mfano mzuri hapa ni wa Mwanamkiwa ambaye anatamani awe profesa ili naye ajilipizie kizazi kwa kuwatesa wanafunzi wake. Kwa jumla hali tete ya masomo idarani inaelekea kuibua uwezekano wa kuiga uovu na ubaya wa wahadhiri wabaya. Wahadhiri hao wana sifa ya ubaguzi, ubinafsi, majitwezo, ulafi, ufisadi, udhalimu, hila na uhinifu miongoni mwa maovu mengine. Tunayashudia haya kupitia kwa kigwena cha mwenyekiti. Mwenyekiti anawapenda na kuwastahi sana kama watu wake anapowahutubia huku akidai ni wakati wao sasa wa kutamba na kula. Anasema:

***Kwenye kigwena cha mwenyekiti wa idara. Washirika wake ambao ni wahadhiri idarani wanaomuunga mkono ambao wengi wao ni wakuu wa kamati mbalimbali za idara wamekutanika kupanga mambo na masuala mbalimbali chini ya uelekezi wa mwenyekiti.***

MBABE: Karibuni na asanteni kwa kufika kwa kikao cha leo ambacho natumahi kitakuwa kifupi kwa sababu mimi nina mkutano wa 'Senate' unaoanza kwa muda mfupi ujao. Naomba mmoja wetu atufungulie kwa maombi. ***(kimya Mwalimu Mgobo anajitolea kuwaongoza kwa maombi ya ufunguzi, anadodosa maombi hayo kwa njia inayodhihirisha hakuwa na uhakika kuhusu kiini cha kigwena chenyewe. Maombi yanapokamilika, kila mmoja anaitikia kwa 'Amina')***

MBABE: Natoa shukrani zangu za dhati kwenu nyote watu wangu. Ninapowaita watu wangu, ninafanya hivyo kwa mazingatio kwani kama mjuavyo, akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki. ***(kimya)*** Mliposimama nami dhidi ya mahasidi wangu mlinifaa. Isitoshe, kwa kuwa safari ingali ndefu, tutazidi kuandamana na kuambatana unyo unyo, *mundu khu mundu* hadi

mwisho. ***(kimya)*** Ninyi ndio masikio yangu, macho yangu na kinywa changu. Ninyi ndio nyundo yangu na zana zangu za vita hii. Ushindi wangu utakuwa ni ushindi wenu. Vita vyangu vitakuwa vyenu, na safari yangu itakuwa safari yenu. ***(kimya)*** Ni wakati wetu sasa wa kusema na kuelekeza sera na utawala wa idara. Mla ni mla leo… waliosema jana na kushamiri na jana, tumekwisha wakamata na kuwadhibiti! Tumekwisha waangusha na kuwabwatabwata. Tumekwisha wasagasaga na kuwabwaga! Nani kama sisi? ***(wote wanapiga makofi na kushangilia hotuba ya Bosi wao)*** Haya sasa nataka nisikie mlivyoshinda adui zetu kwa awamu ambayo imepita, mmoja baada ya mwingine. ***(kimya)*** tuanzie kwa Rafiki wangu wa tangu na tangu Makongoro (***akimwashiria Daktari Makongoro)***

MAKONGORO: Asante sana Boss kwa kunipa fursa hii. Mimi husema daima kwamba wembe ni ule ule! Na kazi ya wembe ni kunyoa, kunyoa na kunyoa. Chini ya uongozi wangu, kamati ya mgao imehakikisha imewafaidi marafiki kwa kazi za ufunzaji wa kozi za ziada na za kulipwa. Kila shujaa wako alipokea kozi tatu za kufundisha ambazo alilipwa na chuo na hivyo kuboresha hali zao za kifedha wakati huu mgumu wa kiuchumi. ***(kimya)***

MBABE: Ulitumia mbinu ipi kutekeleza na kuhifadhi siri, kwani penye kuku wengi…?

MAKONGORO: Mbinu rahisi Boss. Akili! Nilitumia akili. Akili ni mali Bwana. Nilitangaza theluthi moja ya idadi yote ya kozi za ziada kila mara huku nikiwaonya walimu kuwa kozi zilikuwa chache na huenda wengine wasipate kozi yoyote ile. Hili lilifanya wahasidi wengi kufa moyo na kutojihusisha na uombaji wa kozi hizo, wakiogopa kuaibika kwa kukosa kupata. Halafu baadaye nikapakuwa chungu kizima na kuwalisha washujaa. Wakala wakashiba ha!

MBABE: Mbinu hizo lo! Wewe ni shetani kweli kweli. Mbedui wa wabedui wote. Mkala mkasaza. Yakabaki makongoro tu! Anacheka kwa kejeli**. *(kriya)*** Na Makuruhu je ni vipi clientele ukurutu na ukuruhu wako mara hii?

Tunamwona mbabe jinsi alivyojifunga masombo na kusimama kidete kuhakikisha utawala wake dhalimu unaendelezwa na kudumishwa idarani. Anatumia vibraka na vibarakala wake ambao ni wahadhiri waliofuzu kikamilimu na ambao wanajua lililo jema kutendwa ila kinyume na hayo wamegeuka na kuwa majitu yasiyokuwa na huruma. Mbabe anawaita 'watu' wake yaani watu wanaofanya kazi ya ujalibosi pasina kutumia akili zao wenyewe. Wanaridhia na kuitikia kila anachosema bosi wa na kutekeleza kikasuku.

Wamegezwa vizuu na vikaragozi vya kumtumkia bwana wao. Akisema waende kulia au kushoto, wanaende bila ya swali. Anawaita vilevile marafiki wake. Hili linawafanya kujisikia vyema wanaposhirikiana naye kutekeleza maovu dhidi ya "mahasidi" wao idarani. Anawaita vilevile macho na masikio yake. Kazi yao ni kutazama na kusikia kila kinachoonekana na kinachosemwa na maadui wao na kumpelekea mkubwa wao habari. Hili linadhihirisha walivyoshuka chini kimaadili na kifalsafa hadi kutekeleza wajibu sawa na wa mtu ambaye hakwenda shule hata siku moja kusoma.

Kadhalika, Mbabe anawaita 'Nyundo' yake. Hapa ana maana kwamba ni hao hao washirika wake wanaotekeleza miradi yake ya kuhujumu wenzao na watu wengine pale idarani. Washirika hao ndio fimbo inayochapa ya Mbabe. Hili la kuchapa tunaliona likitokea kwa viongozi mbalimbali wa vitengo tofautitofauti idarani kutokana na wanayokiri wenyewe katika kigwena hicho. Wa kwanza na Prof Makongoro ambaye ndiye mwenyekiti wa kamati ya mgao wa kazi idarani. Anatumia hila na njama kutekeleza kazi yake kwa kupendelea upande wa Mbabe. Hili linapelekea kwa wao kujipatia mtaji kutokana na mafunzo ya ziada

*Journal of African Interdisciplinary Studies (JAIS)*: **ISSN 2523-6725** (online)
**October 2024 Vol. 8, No. 10**
**Citation**: Jeptanui, S & Gakuo, J. K. (2024). Usawiri Wa Changamoto Zinazowakumba Wazamilifu Katika *Ubabe. Journal of African Interdisciplinary Studies,* 8(10), 405 – 420.

pale idarani wakati wapinzani wao wakila mwande. Kamati zote zina hujuma humo idarani. Kuna pia, kamati ya Safari za nyanjani, kamati ya jarida la idara, kamati ya masilahi na kamati ya uzamilifu. Kamati zote hizi zinatekeleza amri ya upunjufu na udhalimu wa Mbabe dhidi ya mapinzani wao wakiwemo wanafunzi wanaoelekezwa kuhusu utafiti na wahadhiri wa upande kinzani. Hili nalo linakuwa na athari kubwa kwa wazamilifu. Linawafanya wengine wao kutotaka kuendelea na taaluma husika

Wawili hao wanashurutishwa kurejelea mada zao za awali walizoachana nazo kutokana na uamuzi wa idara. Inadhihirika kwamba tayari wawili hao wameandaa mada mpya za utafiti na kuyasahau ya nyuma. Hata hivyo, inawalazimu kufuata ushauri wa wengi kwani wengi wape… hili linaudhi na kuumiza nyoyo sana. Katika kifungu hiki vilevile tunapata habari za janga la Uviko 19 yaani Korona. Inadhahiri kwamba tamthilia hii iliandikwa wakati janga hilo lilikuwa linatesa dunia nzima. Ni wazi kwamba vyuo vingi vya masomo vilifungwa kutokana na hatari ya ugonjwa huu na kwamba vyuo vikuu kwa kuwa havikuwa na sera yoyote ya kukabiliana na gonjwa hilo, vilitegemea ushauri na uelekezo wa wizara ya afya. Tunatambua hapa pia licha ya changamoto za masomo zilizosababishwa na idara kwa wazamilifu hawa na wenzao, wawili hawa walikuwa wanafunzi bora wa kiwango cha A masomoni.

Kikao hiki kinakuwa mwanzo tu wa vikao vingi vingine. Wanajikuta kwa vikao vingi vya ziada. Wawili hao wanalazimika kukutana na wasimamizi wao wa zamani pamoja na wasimamizi wengine wapya. Hili nalo linawaweka kwenye mzunguko usiokuwa na kifani.Wanachukuwa muda mrefu kuzungukia maswala yale yale ambayo tayari walishashughulikia zamani na kuwafanya kuwa na kazi za ziada bure bilashi. Mahiri na Mwanamkiwa wanashughulikia mada mpya ambazo baadaye haziendelezwi kamwe na kulazimika kurejelea yote waliokwisha kusahau na kuanza upya au kuendelea mbele. Wakati huo huo, wasijue kama ndio mwazo mkoko unaalika maua au ndio mwanzo mwanzo wa mwisho wa safari yao ya masomo unaanza.

**1.4 Hitimisho**

Makala haya yamejizatiti kuchunguza changamoto zinazowakumba wasomi wa ngazi za juu zaidi katika vyuo vikuu Kenya na kwingineko duniani.Changamoto zinazowakumba wazamilifu ni nyingi kama tulivyodokeza hapo juu. Baadhi ya changamoto hizo kama tulivyoona zina madhara mengi ya kijamii kiafya, kiuchumi na hata kimstakali kwa wasomi hao ambao ndio mhimili wa uendelevu wa taaluma anuai nchini na duniani kote. Changamoto hizi zafaa kusuluhishwa ili kuboresha masomo ya shahada za juu. Ni kweli kama tulivyodokeza kwamba wasomi wa kiwango cha juu ndio wataalamu wa kesho. Uzamilifu hivyo basi ni kiungo cha uendelevu wa taaluma anuai zinazosomewa katika vyuo vikuu nchini na kwingineko. Baadhi ya changamoto hizi zinaweza kutatuliwa ila zingine ni za kimfumo ambazo zinahitaji kuudurusu na kuurekebisha mfumo mzima wa utawala vyuoni. Zingine zinahitaji upigaji msasa na uimarishaji wa asasi mbalimbali za jamii nzima. Ni matumaini yetu kwamba makala haya yatakuwa kihamasisho kwa wadau mbalimbali kutafakari na hatimaye kuibua tatuzi ya matatizo ya changamoto hizo zilizo tisho kubwa kwa elimu nchini na kwingineko duniani.

**Marejeleo**

Chepkoech, S. (2018), *Usawiri wa Maudhui yenye kufunza Wanafunzi wa Vyuo Maadili Mema: Tathmini ya Alidhani Kapata na Damu Nyeusi*, Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Kenyatta, Haijachapishwa.

Gakuo J. (2020) *Ubabe* Globe Edit, Amazon, Germany.

Lukacs, G. (1963), The Meaning of Contemporary Realism. London: Merlin Publishers

Kairi, A. (2014), *Ukoloni Mamboleo na Utandawazi katika Tamthilia Teule*, Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Kenyatta, Haijachapishwa.

Kibet, E. (2016), *Usawiriwa Vijana katika Tamthilia ya Mbaya Wetu*, Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Kenyatta, Haijachapishwa.

Kahara, I. (2011), T*amthilia kama Utendi: Uchanganuzi linganishi wa Tamthilia za Kinjeketile na Mzalendo Kimathi*, Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Kenyatta, Haijachapishwa.

Mahero, A. (1992), *Maono ya Jamii katika Tamthilia za Chacha Nyaigoti Chacha (Suala la Uongozi)*, Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Kenyatta, Haijachapishwa.

Otoro, m. A. (2012). *Msimbo na maana katika tamthilia ya zilizala* (doctoral dissertation, university of nairobi, kenya).

Masoud, A., & Omary, M. (2022). Maudhui yanayojitokeza katika tamthilia ya kaptula la marx kupitia tashtiti. *Journal of human sciences*, *21*(2), 131-137.

Mule, K. (1991), *Suala la wanawake katika Tamthilia ya Kiswahili: Waandishi wa kike katika njia Panda*, Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Kenyatta, Haijachapishwa.

Musyoka,T. (2008), *Usawiri wa Vijana katika Tamthilia Teule za Kiswahili*,Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Kenyatta, Haijachapishwa.

Njogu, K. na Chimera, R.. (1999), Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu, Nairobi JKF

Okwena, S. (2013), *Matumizi ya Jazanda katika Tamthilia Tatu za Timothy Arege*, Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Kenyatta, Haijachapishwa.

Wamitila K. (2002), Uhakiki wa fasihi, Misingi na Vipengele vyake, Nairobi: Phoenix Publishers